OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# JARIDA

## LA MWEZI WA SABA

*Tolea la kwanza 2024*

WELEDI NA UBORA

# NENO LA UKARIBISHO KUTOKA KWA MHARIRI

Karibuni sana wasomaji wetu katika toleo letu la kwanza la Jarida hili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaongozwa na Dira ya kuwa Taasisi yenye ufanisi kitaaluma na kuaminika katika kutoa huduma bora za kisheria kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Dhamira yetu ni kutoa huduma za kisheria zenye ubora kwa njia ya kuandaa Sheria, Upekuzi na Majadiliano ya Mikataba pamoja na Ushauri wa Kisheria kwa Maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa.

Kwa sababu hiyo basi, kuanzishwa kwa Jarida hili ambalo litakuwa likitoka mara moja kila mwezi, kunalenga kupeana taarifa, kupashana habari, kufahamishana na kuelimishana kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan kupitia Divisheni na Vitengo. Tunaamini kabisa kuwa, litachangia sana katika kuwafanya ninyi wasomaji wetu na wadau wetu kwa ujumla kufahamu kwa kina ni yepi majukumu ya Ofisi yetu, tukiwa kama washauri Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yote ya kisheria.

Kupitia Jarida hili, tutaweza kuainisha mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yetu, lakini pia tunaamini kadri tutakayokuwa tukiendelea, mtaweza pia kulitumia kama hadidu ya rejea kutokana na taarifa mbalimbali zitakatokuwa zinatolewa ndani ya Jarida hilo hususan masuala ya kisheria pamoja na kufahamu kazi ambazo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inafanya.

Aidha, ndani ya Toleo hili la kwanza la Jarida la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunakuletea makala na habari mbalimbali ikiwemo pamoja na mambo mengine, Mkutano wa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mafunzo maalum yaliyotolewa kwa Mawakili wa Serikali na habari zingine nyingi.

Vilevile, toleo hili linajumuisha matukio muhimu yaliyofanyika katika kipindi chote cha toleo husika, ambapo pamoja na mengine ni tukio muhimu la wiki ya kliniki ya utoaji wa ushauri na elimu ya bure ya sheria iliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square, Jijini Dodoma na kuzinduliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi. Kliniki hii ni endelevu na jitihada zinaendelea ili kuhakikisha wananchi wa mikoa mingine wanafikiwa na kunufaika pia na huduma hii ya bure itakayosaidia kuzipatia ufumbuzi changamoto na migogoro mbalimbali ya kisheria inayowakabili wananchi na kuhakikisha wanapata haki stahiki.

Haya ni masuala machache tu ambayo tunaamini mtanufaika nayo ndani ya jarida hili,.Hivyo basi, kwa mara nyingine tena, Nichukue fursa hii kuwakaribisheni wote kusoma yale tuliyowaandalia katika Jarida hili la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, toleo la Julai, 2024. Ninyi wasomaji wetu ni sehemu muhimu ya mafanikio yetu, hivyo basi msisite kutoa maoni yenu ili kuendelea kuboresha jarida hili.

Nitumie fursa hii kuwashukuru wale wote waliofanikisha maandalizi na hatimaye kukamilika kwa Jarida hili la kwanza. Ni matarajio yetu tutakidhi kiu yenu.

Ahsanteni na Karibuni sana

# MHE. SAGINI AKOSHWA NA UTOAJI WA ELIMU KWA WANANCHI

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini, amefurahishwa na jitihada zinazofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali za kutoa elimu na ushauri wa Kisheria kwa Wananchi. Mhe Sagini aliyasema hayo wakati alipotembelembea kliniki ya bure ya ushauri wa Kisheria iliyoandaliwa na kuratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano na Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania.

Mhe Sagini alipongeza uamuzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kuanzisha Kliniki hiyo huku akiamini itakuwa msaada mkubwa kwa Wananchi, *"Nipongeze kwa kuanzishwa kwa jambo hili kipekee nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi kwa kuja na mawazo haya, ni matumaini yangu jambo hili litawasaidia wananchi wengi wenye changamoto za Kisheria"..*

Katika hatua nyingine Mhe. Sagini aliwaagiza Maafisa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kutoa elimu na Ushauri wa Kisheria huku akisisitiza suala hilo kuwa endelevu na kufanyika kwenye maeneo mengi nchini. *"Niwaombe muendelee kutoa ushauri wa kisheria kwa umma, mjitahidi muwafikie wananchi wengi na hili jambo liwe endelevu pia msiishie Dodoma tu muendelee na maeneo mengine nchini".*

Katika kliniki hiyo ya huduma za bure za kisheria, Wananchi wengi waliweza kujitokeza na kupata huduma za Ushauri na msaada wa Kisheria pamoja na masuala ya ardhi, mirathi na ndoa.
Aidha, mipango ya baadae ni kuhahakikisha wananchi wengi zaidi wanahudumiwa kupitia Kliniki ya Sheria Mikoani.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini (Kulia) akimsikiliza mmoja wa Wananchi waliojitokeza kwenye Kliniki ya Huduma za Sheria iliyoratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Jijini Dodoma hivi karibuni.*

# MHE. SAGINI ASISITIZA USHIRIKIANO KWA WATUMISHI NA UTATUZI WA CHANGAMOTO KWA WANANCHI

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini ameipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria katika utatuzi wa changamoto mbalimbali pamoja na kutoa huduma bora za kisheria kwa wananchi na Serikali kwa ujumla.

Mhe. Sagini ameyasema hayo, mara baada ya kukutana na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mkoani Dodoma hivi karibuni, ambapo amewataka watumishi hao kuendelea kushirikiana huku kila mmoja akitakiwa kuyajua na kuyatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Aidha, Mhe. Naibu Waziri amewataka watumishi kuendelea kushikamana na kushirikiana katika maeneo yao ya kazi, na pale kunapobainika kuwepo kwa baadhi ya changamoto baina yao, watafute njia bora ya kuzitatua bila kuathiri utendaji wa kazi.

*"Lengo letu ni kuwezesha Sekta yetu kupata mahitaji yatakayoweza kusaidia kufanikisha majukumu muhimu kwa Wananchi na Serikali katika ubora na ufanisi mkubwa".*

Mhe. Naibu Waziri alipongeza juhudi na ubunifu uliofanywa wa kuwa na Kliniki ya elimu ya sheria ambayo imelenga kutatua changamoto za kisheria wanazokabiliana nazo wananchi na hatimaye kupata haki stahiki.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria mkuu wa serikali katika mkutano kati yake na Watumishi hao uliofanyika hivi karibuni Jijini Dodoma.*

Awali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Balozi Prof. Kennedy Gastorn akisoma taarifa fupi kwa Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Sagini na kutaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na jumla ya sheria 300 zimefanyiwa tafsiri kwa lugha ya Kiswahili, huku sheria hizo zikisubiriwa kutangazwa katika toleo la Urekebu.

Akifafanua zaidi, Mhe. Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametaja mambo kadhaa ambayo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikisha kuandaa hadi sasa kuwa ni pamoja na maazimio kumi ya kuridhia mikataba na itifaki mbalimbali yaliyoandaliwa na kuwasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*"Tumeweza kutoa mafunzo mahsusi kwa waandishi wa Sheria, Majadiliano ya Mikataba, na utoaji wa ushauri kwa mawakili 300 wa Serikali kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali ambao wameweza kushiriki katika Mafunzo hayo."*




*Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Balozi Prof. Kennedy Gastorn akifafanua jambo wakati wa kikao kati ya Naibu Waziri wa Katiba Sheria na Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kilichofanyika Jijini Dodoma.*

## *Baadhi ya matukio katika picha*





# JAJI MKUU AISIFU OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KUTAFSIRI SHERIA

Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof Ibrahim Hamis Juma hivi karibuni ametembelea Maonesho ya Sabasaba na kuzungumza na Maafisa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali waliokuwa wakitoa huduma za Kisheria kwa Wananchi.

Akiwa bandani hapo, Mhe. Jaji Mkuu alisifu jitihada za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali za kuamua kutafsiri Sheria mbalimbali na kuwa lugha ya Kiswahili huku akishauri kuwa ni muhimu, baada ya Sheria hizo kufanyiwa maboresho ziwe zinapatikana kwa lugha ya Kiswahili na Kingereza.

Akitoa maelezo kwa Mhe. Jaji Mkuu, Wakili Mwandamizi wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Angella Kimaro alisema sheria hizo zitapatikana kwa lugha ya Kiswahili na Kingereza. *"Sheria hizi Mhe. Jaji zitapatikana kwa lugha zote mbili kupitia mifumo yetu, pia wananchi wataweza kuziona Sheria zilizofanyiwa marekebisho kupitia madirisha yaliyoko kwenye mifumo yetu"*.




*Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma akisikiliza maelezo yaliyokuwa yanatolewa na Maafisa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipotembelea banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye Maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

# MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AZINDUA KLINIKI YA BURE YA SHERIA KWA KUSIKILIZA KERO ZA WANANCHI

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi amezindua rasmi Kliniki ya huduma za bure za kisheria katika viwanja vya Nyerere Square Jijini Dodoma.

Kliniki hiyo iliyoandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Mawakili wa Serikali ni utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kutaka Viongozi kuwa na utaratibu wa kusikiliza malalamiko ya wananchi ikiwa ni pamoja na kuwaongoza katika taratibu za kupata haki.

Akizindua Kliniki hiyo hivi karibuni Jijini Dodoma, Dkt. Feleshi amesema Kliniki itasaidia kusogeza msaada wa huduma za kisheria kwa wananchi na kutatua changamoto mbalimbali zinazohusu sheria.

Katika hatua nyingine, Jaji Feleshi ametoa maagizo kwa Mawakili wa Serikali kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii na kutatua kero za wananchi *"Natoa rai kwa Mawakili wote wa Serikali hapa nchini kutenga muda na kusikiliza kero mbalimbali za wananchi kwa kuwatembelea kwenye maeneo yao".*

Aidha, aliwaomba pia Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambao bado hawajakamilisha kuteua wajumbe wawili wa Kamati za Ushauri wafanye hivyo ili Kamati hizo zianze kusikiliza malalamiko ya wananchi kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa.

Katika Kliniki hiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt Eliezer Feleshi alipata wasaa wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi waliotembelea kwenye mabanda mbalimbali ya huduma za sheria yaliyokuwepo viwanjani hapo.





*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi akizungumza wakati wa ufunguzi wa Kliniki ya huduma za Kisheria iliyoratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Viwanja vya Nyerere Square, Jijini Dodoma.*

## / *Baadhi ya picha katika ufunguzi wa kliniki ya sheria*









# MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AWAKARIBISHA WATUMISHI WAPYA

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, amefanya kikao na Watumishi wapya walioajiriwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kikao hicho kililenga kuwakaribisha Watumishi hao katika Ofisi hiyo na kilifanyika katika Ukumbi wa Msekwa Bungeni, Jijini Dodoma.

Akizungumza wakati wa kikao hicho Mhe. Mwanasheria Mkuu aliwakaribisha Watumishi hao, huku akiwaahidi ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao, *"Kwanza nianze kwa kuwakaribisha sana kwenye Ofisi hii mjisikie huru kuuliza mambo mbalimbali na binafsi nawaahidi ushirikiano mzuri kutoka kwangu na hata wakuu wa Divisheni, Vitengo na Watumishi naamini watawapa ushirikiano*".

Aidha, alisisitiza suala la uwajibikaji na kujituma kwa Watumishi hao, ambapo alisema imani yake kubwa ni kuwa Watumishi hao watafanya kazi kwa bidii na kufuata misingi na weledi ili kuleta mafanikio kwenye Ofisi hiyo. *"Nawaomba mfanye kazi kwa bidii na kufuata weledi na ubora, ni matumaini yangu mtakuwa chachu ya mafanikio ya Ofisi hii".*

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali alimalizia kwa kuwatakia kila la kheri Watumishi hao kwenye Utumishi wao katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na matarajio yake ni kuwa ujio wao utaongeza kasi ya Utendaji Kazi wa Ofisi hiyo.



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, akizungumza wakati alipofanya kikao na Watumishi wapya waliojiunga na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hivi karibuni.*

# OFISI YA MWANASHERIA MKUU YASIFIWA KUTOA MIONGOZO YA SHERIA

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi Mhe. Jaji Dkt. Yose Joseph Mlyambina ameipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutoa Miongozo mbalimbali ya Kisheria.

Mhe. Mlyambina ameyasema hayo alipotembelea banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika hivi karibuni Jijini Dar es Salaam, ambapo amesema miongozo hiyo itawasaidia wadau mbalimbali wa sheria. *"Niwapongeze kwa kutoa miongozo hii, ni imani yangu sasa wadau wa sekta ya sheria wataifuata miongozo na itawasaidia katika kuboresha utendaji wao wa kazi"*.

Pia alipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kutoa Jarida maridhawa lijulikanalo kama *Brain behind legislative Drafting in Tanzania*.

*"Niwapongeze pia kwa kuanzisha jarida hili natumaini wananchi hasa wadau wa sheria watajifunza mengi kuhusu nyinyi kupitia jarida hili."*

Awali akimkaribisha Mhe. Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Wakili wa Serikali Mwandamizi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Angella Kimaro alieleza kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imetoa Miongozo na nyaraka mbalimbali.

Miongozo iliyotolewa ni kama vile Mwongozo wa utoaji wa ushauri wa Kisheria, Mwongozo wa Mikataba, Mwongozo wa Kamati za ushauri wa Kisheria za Wilaya na Mikoa, Mwongozo wa utengenezaji wa Sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mwongozo wa Uandishi wa Sheria. Pamoja na Miongozo hiyo Ofisi pia imetoa majina ya Sheria kwa lugha ya kiswahili, na istilahi za Kisheria, nyaraka hizi zinalenga kuboresha utendaji kazi katika Sekta ya Sheria.




*Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi Dkt. Yose Joseph Mlyambina (Kushoto) akisilikiza maelezo kutoka kwa Mawakili wa Serikali wakati alipotembelea banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika Jijini Dar es Salaaam.*

# MWANDISHI MKUU WA SHERIA ATEMBELEA BANDA LA OFISI YA MWANASHERIA MKUU SABASABA

Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole alikuwa mmoja wa Viongozi waliotembelea Banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Akiwa katika banda hilo Bw. Njole alipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushiriki kwenye maonesho hayo, huku akisema ni hatua nzuri kwa Ofisi hiyo katika utoaji wa elimu kuhusu masuala mbalimbali ya Kisheria kwa wananchi.

*"Muitumie hii nafasi kuwapa elimu wananchi juu ya masuala ya Sheria na muhakikishe kuwa wanajua mambo mbalimbali tunayoyafanya na pia muendelee kutoa ushauri wa kisheria ili kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi".*

Mwandishi Mkuu wa Sheria aliambatana na Wakili wa Serikali na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar Bi. Fatma Ally



*Mwandishi Mkuu wa Sheria Bw. Onorius Njole (kulia) akizungumza na Mkurugenzi wa Rasimali watu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar Bi. Fatuma Ally, wakati wa maonesho ya Sabasaba yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam, katikati ni Maafisa wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kushoto ni Wakili wa Serikali Bi. Angella Kimaro na kulia ni Wakili wa Serikali Bw. Emmanuel Mwaikambo.*

## *Matukio ya picha katika Maonesho ya Sabasaba*













# DIVISHENI YA URATIBU NA USHAURI WA KISHERIA YAFANYA KIKAO KAZI

Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Neema Ringo ameongoza kikao cha Divisheni hiyo kilichofanyika hivi karibuni katika ukumbi wa mikutano wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jijini Dodoma.

Kikao hicho kililenga kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Divisheni hiyo ikiwemo namna bora ya kutekeleza majukumu ya Divisheni, kujengeana uwezo kwa Watumishi wa Idara hiyo na matumizi bora ya mfumo wa mawakili unaotumiwa na Divisheni hiyo.
Aidha, Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria aliwasisitiza Watumishi wa Divisheni hiyo kujaza taarifa zao za utendaji kazi kwenye mfumo wa PEPMIS kwa wakati.

*"Niwasisitize mjaze taarifa zenu za utendaji kazi wenu kwenye mfumo wa PEPMIS kwa wakati, na hivi sasa mfumo umezinduliwa rasmi hivyo tunaamini utakuwa vizuri na watumishi wa Divisheni yangu mnatakiwa kujaza kazi zenu kwa wakati".*

Kikao hicho kilifanyika na kuwahusisha Watumishi wote wa Divisheni hiyio walioko Jijini Dodoma na wengine walioko mikoani walishiriki kwa njia ya mtandao.





*Watumishi wa Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria wakiwa kwenye kikao cha kujadili utendaji kazi wa Idara hiyo hivi karibuni, kikao hicho kilifanyika katika Ukumbi wa Ofisi za Mwanasheria Mkuu Mtumba Jijini Dodoma.*

# WATUMISHI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI WASHIRIKI BONANZA LA MICHEZO

Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wameshiriki kwenye Bonanza la Michezo liliofanyika katika Viwanja vya Kilimani, Uzunguni Jijini Dodoma.

Watumishi hao wakiongozwa na Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi Regina Mutagurwa, walishiriki michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, drafti, karata, kukimbia kwenye gunia na kukimbiza kuku.

Akizungumza kwenye ufunguzi wa bonanza hilo, Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Regina Mutagurwa aliwapongeza Watumishi hao kwa kuhudhuria bonanza hilo, kwani kufanya hivyo ni kuimarisha afya zao, pia aliwataka kutumia fursa hiyo kama sehemu ya kujenga ushirikiano na furaha baina ya Watumishi.

*"Nawapongeza nyote kwa kuja kwenye bonanza hili, sote tunatambua michezo ni afya na furaha, niwaombe mtumie bonanza hili kama sehemu ya kuimarisha umoja na ushirikiano wetu, Nawatakia michezo mema".*

Bonanza hilo liliisha kwa Watumishi kutoka Divisheni na Vitengo kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushinda zawadi mbalimbali kama vile Vikombe na fedha taslimu .



*Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Regina Mutagurwa, akikabidhi kikombe kwa mmoja wa Washindi katika Bonanza la Michezo lililowashirikisha Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.*

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA

WELEDI NA UBORA

PROFESSIONALISM & EXCELLENCE

THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

# MAKALA MAALUMU ZA MAFUNZO (6 – DAY BESPOKE TRAINING) KWA MAWAKILI WA SERIKALI YALIYOFANYIKA MEI HADI JUNI 2024

# MATUMIZI YA TEKNOLOJIA KATIKA KUBORESHA UTOAJI HAKI




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo maalumu kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Dodoma.

Hivi karibuni dunia imeshuhudia mabadiliko makubwa katika nyanja za teknolojia, mojawapo ya teknolojia inayokuwa kwa kasi ulimwenguni kwasasa ni akili bandia (artificial intelligent), teknolojia hii imeleta mageuzi makubwa katika utendaji kazi wa kada mbalimbali. Ukuaji huu wa teknolojia hususan matumizi ya akili bandia ni moja ya maeneo yaliyozungumzwa kwenye Mafunzo Maalumu kwa Mawakili wa Serikali yaliyoandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambapo Mgeni Rasmi katika Mafunzo hayo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene alisema kuna umuhimu wa kuingia katika matumizi ya akili bandia ili iwasaidie kulinda uaminifu na taaluma.

Ni muhimu kwa Mawakili kuzingatia na kuingia katika utumiaji wa teknolojia ya akili bandia ili kuhakikisha kada ya sheria inakwenda sambasamba na mabadiliko ya teknolojia katika utoaji wa huduma bora za kisheria. Mhe. Simbachawene ametoa rai hiyo alipoalikwa kama mgeni rasmi wa ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Dodoma mwezi Juni 2024. Pia aliwataka Mawakili kuzingatia kasi ya ukuaji wa teknolojia katika utoaji wa huduma za kisheria, huku akiyataja matumizi ya teknolojia ya akili bandia kuwa yataongeza kasi na ubora katika kazi zao kwakua teknolojia hiyo inakuwa kwa haraka duniani. *"Akili ya kibinadamu, mawazo ya kibinadamu pekee yake yanaweza kutuchelewesha kwa sababu dunia inakwenda kwa kasi, hivyo akili bandia haiepukiki katika utendaji wetu."*

Pamoja na kusisitiza matumizi ya akili bandia, Mhe. Simbachawene amewataka Mawakili kutengeneza mtandao wa ushirikiano na vyombo vingine vya kisheria, asasi za kiraia na mashirika mengine ili kuhakikisha wanaboresha mfumo wa sheria kwa manufaa ya wananchi wote. Aidha, ameendelea kuwakumbusha Mawakili wajibu wao kwa Jamii ambapo amesema Mawakili wanawajibu wa kulinda maslahi ya umma kwa kuhakikisha kuwa wanazingatia utendaji wa haki kwa Serikali, kusimamia kesi za Serikali na kuhakikisha kuwa shughuli zote za kuijenga Serikali zinafanyika kwa kufuata misingi ya sheria.

Aidha, amewataka Mawakili kuzingatia utawala bora, huku akiwakumbusha umuhimu wa kuzingatia haki za watu na za Serikali na kwamba kuna wakati haki hizo zinagogana. Akirejea mfano wa mwanafalsafa wa kirusi na kimarekani aliyeishi mwaka 1905 hadi 1982 ambaye alisema *"Serikali iliundwa ili kuwalinda watu dhidi ya wahalifu huku Katiba ikiundwa kumlinda watu dhidi ya Serikali."*

Mhe. Simbachawene amewataka Mawakili wa Serikali kuzingatia mizania ya haki katika kuamua haki za watu na Serikali. Pia alihimiza matumizi ya teknolojia ikiwemo matumizi ya akili bandia na kwamba anaamini matumizi sahihi ya teknolojia ya akili bandia itawasaidia kwa kiasi kubwa Mawakili katika kulinda haki za wananchi pamoja na Serikali.

# MAWAKILI WA SERIKALI WAFUNDWA JUU YA UTATUZI WA MASHAURI YA MADAI DHIDI YA SERIKALI

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imewafunda Mawakili wa Serikali kuhusu utatuzi wa mashauri dhidi ya Serikali yanayofunguliwa katika Mahakama mbalimbali nchini. Hayo yalielezwa wa wakati mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyoandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyofanyika hivi karibuni.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo Mgeni Rasmi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene, Alisema kuwa mara kadhaa amepokea malalamiko ambapo wananchi wameshinda dhidi ya Serikali kuanzia ngazi ya Mahakama ya Wilaya hadi Mahakama kuu, lakini Mawakili wa Serikali wanakata Rufaa dhidi ya maamuzi hayo.

Aliendelea kusema kufanya hivyo sio utawala bora wa sheria, pia aliwakumbusha Mawakili wa Serikali kuwa moja ya majukumu yao ni kulinda haki za watu na Serikali. *"Ni muhimu mkafahamu kuwa ninyi mmebeba dhamana ya kutetea haki za Watanzania, mnapaswa kuangalia mizania ya haki na si kuangalia ushindi tu kwa Serikali*".

Aidha, Mhe. Simbachawene alirejea kauli ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa Chama cha Mawakili wa Serikali (TPBA) aliposema kwamba *"Mawakili ni Jeshi la ulinzi wa uchumi wa nchi kwa kutumia kalamu zao".* Kauli hii inasisitiza nafasi kubwa ya Mawakili wa Serikali katika kuimarisha Utawala bora. Kwa upande wake Wakili Mkuu Mstaafu wa Serikali Dkt. Clement Mashamba alieleza masuala ya msingi ya kuzingatiwa na Mawakili wa Serikali ili kuhakikisha wanapunguza mashauri dhidi ya Serikali kwa kuhakikisha kwamba Idara na Kurugenzi za Huduma za Sheria zinakuwa mwongozo wa namna ya kushughulikia migogoro na mashauri ambayo yanaweza kujitokeza.

Alisisitiza kuwa lazima sehemu husika za huduma za sheria ziwe na utaratibu wa ndani wa kudhibiti mashauri, pia alishauri kuwa na utaratibu wa kufanya marejeo ya miongozo mbalimbali mara kwa mara ili kuendana na wakati.

Aidha, Dkt. Mashamba aliongeza kusema kuwa kama Serikali kupitia wanasheria wake inapaswa kuwa na mfumo wa kisheria ambao umezingatia sheria za biashara na uwekezaji kimataifa. Pia wanasheria wanapaswa kufanya majadiliano ya kina kabla ya kuingia makubaliano yoyote.

Dkt. Mashamba alisisitiza kwamba wanasheria wanapaswa kujiendeleza katika maeneo mapya ya kisheria kwa kuongeza ujuzi, kufanya mafunzo na tafiti mbalimbali za masuala ya kisheria na kutoa elimu kwa Umma.

Kwamba upande wake Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende aliwasisitiza Mawakili wa Serikali kuongeza umakini na kuhakikisha pindi wanaposaini Mikataba wanapaswa kuipitia kwa kina, aliongeza kusema kwamba usimamizi mzuri wa mikataba utaiepushia Serikali mashauri au migogoro isiyo na tija.

Aliwahimiza Mawakili wa Serikali kuwa wanapaswa kujibu kila notisi wanayotumiwa na wadau au wazabuni ili kuepusha migogoro ambayo hupelekea wazabuni hao kwenda Mahakamani.

Aidha, aliwakumbusha siku zote kuendelea kufanya mapitio ya kesi zao kabla na baada ya kuwasilishwa Mahakamani, endapo watabaini hakuna nafasi ya Serikali kushinda basi ni vyema kufanya mazungumzo ili kupata usuluhishi nje ya Mahakama.

# MAWAKILI WA SERIKALI WASHIRIKI MAFUNZO YALIYOANDALIWA NA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi akizungumza wakati wa mafunzo maalumu kwa Mawakaili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (OMMS) iliandaa mafunzo ya siku sita (6) kwa Mawakili wa Serikali. Mafunzo hayo yalifanyika katika Ofisi za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali jijini Dodoma. Lengo la mafunzo hayo ni kukuza uwezo wa Mawakili wa Serikali katika utoaji wa huduma bora za kisheria, kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali ili waweze kuendana na mabadiliko yanayoendelea kutokea katika sekta mbalimbali ambayo yamesababisha kuwepo kwa mabadiliko ya sheria na kuimarisha weledi wa Mawakili wa Serikali ili kuhakikisha kunakuwa na utawala wa sheria na utawala bora kwa ajili ya ustawi wa jamii na Taifa kwa ujumla.

Mwitikio wa kuhudhuria mafunzo kwa Mawakili wa Serikali ulikuwa ni mkubwa kiasi cha kufanya Kamati ya uratibu wa mafunzo kubadilisha sehemu ya kufanyia mafunzo hayo. Hata hivyo, jumla ya Mawakili wa Serikali 290 washiriki katika mafunzo na kupewa vyeti vya ushiriki.

Mafunzo haya yalifunguliwa na Mgeni Rasmi Mhe. George Simbachawene, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Hata hivyo, katika hotuba yake ya ufunguzi alieleza kuwa, sheria ndio nyenzo kuu katika upatikanaji wa haki za watu na Serikali, hivyo nchi yoyote ya kidemokrasia lazima izingatie utawala wa sheria na utawala bora.

Katika mafunzo hayo mada na hoja mbalimbali ziliwasilishwa, ziliibuliwa, kujadiliwa na kutolewa ufafanuzi na wataalam wabobevu katika maeneo mbalimbali ya kisheria ikiwemo majadiliano ya mikataba na migogoro ya kitaifa na kimataifa, utoaji wa ushauri wa kisheria na changamoto za mashauri katika mabaraza mahakama za kimataifa,

mbinu zinazotumika kutafsiri sheria, masuala muhimu ya kuzingatia wakati wa kuishauri Serikali, wajibu wa Wakili wa Serikali katika kuzuia na kutatua mashauri ya madai dhidi ya Serikali, mwongozo madhubuti kwenye taratibu za ununuzi wa umma kwa Mawakili wa Serikali, misingi ya uandishi wa sheria, na uandaaji wa sera madhubuti kwa ajili ya serikali kutoa uamuzi.

Baada ya kumalizika kwa mafunzo hayo, washiriki walionyeshwa kufurahishwa na mada zilizowasilishwa pamoja na wawezeshaji wa mafunzo. Baadhi ya washiriki waliendelea kusema *“mafunzo haya yamekuwa na msaada mkubwa sana kwetu Mawakili wa Serikali kwani tumepata fursa ya kujifunza mambo mengi, ni vema yakawekewa utaratibu wa kufanyika mara kwa mara”.*

Hata hivyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi wakati akihitimisha mafunzoa limpongeza Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Menejimenti ya OMMS pamoja na Kamati ya maandalizi kwa kuwezesha kukamilika kwa mafunzo hayo.

*“Nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kamati ya Maandalizi kwa kuandaa mafunzo haya yenye lengo la kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha Mawakili wa Serikali wanawezeshwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.”*

# MAWAKILI WAFUNDWA KUONGEZA WELEDI KATIKA KUTUMIKIA UMMA




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi akisisitiza jambo wakati wa mafunzo ya siku sita kwa Mawakili wa Serikali.*

Hivi karibuni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (OMMS) iliendesha mafunzo maalumu ya siku sita kwa Mawakili wa Serikali, mada mbalimbali kama vile uandishi wa sheria, ufasiri wa sheria, ushauri wa kisheria na upekuzi wa mikataba, zilizotolewa kwa washiriki wa mafunzo hayo.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo hayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, aliwataka Mawakili wa Serikali kuyatumia mafunzo hayo kama chachu ya kuongeza weledi katika kutumikia Umma. Mafunzo hayo yalilenga kuwaongezea ujuzi, ubunifu na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi kwa Mawakili wa Serikali.

Aidha, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliendelea kuwakumbusha Mawakili wa Serikali juu ya wajibu wa kutambua majukumu yao, ambapo alisema.

*"Tunafahamu kuwa kama Mawakili wa Serikali jukumu letu la msingi ni kuishauri na kuiwakilisha Serikali ipasavyo kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mstaafu Mhe. Jaji George Masaju amekuwa akisisitiza".*

Mhe. Mwanasheria Mkuu aliwashauri wakuu wa Wizara na taasisi za Serikali kuwashirikisha Mawakili na Maafisa Sheria katika masuala yote ya kisheria kwenye Ofisi zao ili kuweza kuishauri Serikali na kuepusha migogoro isiyo ya lazima. Katika hatua nyingine Mhe. Feleshi aliongelea juu ya umuhimu wa mafunzo ya uandishi wa sheria kwa sababu yanawajengea uwezo wa kuandaa sheria zinazotekelezeka na vyombo mbalimbali vya utoaji haki. Aliongeza kwa kusema;

*"Naamini mafunzo haya pia yamesaidia kuibua maeneo ambayo tunazani yanahitaji maboresho au kutungiwa sheria na masuala muhimu ambayo yanapaswa kuzingatiwa wakati wa uandishi wa sheria".*

Aidha, aliendelea kuwakumbusha Mawakili wa Serikali juu ya umuhimu wa kuboresha madhumuni na sababu wakati wa kuandaa miswada ya sheria. Hii itawasaidia kuelewa lengo na sababu ya kutungwa kwa sheria au kurekebisha vifungu katika Sheria, huku akiwataka Mawakili kubadilisha mtazamo wa kifikra wakati wa kufanya maboresho ya sheria katika taasisi zao.

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kupitia mafunzo hayo Mawakili wa Serikali watakuwa wamepata uelewa na kujengewa uwezo wakati wa kujadili, kuandaa, kutekeleza, kusimamia na kufanya upekuzi wa mikataba ili kulinda maslahi ya Serikali na wananchi kwa ujumla. Mafunzo yaliyotolewa kwa Mawakili wa Serikali yatasaidia kuhakikisha kuwa mikataba iliyopekuliwa inatekelezwa kwa kuzingatia miongozo ya Serikali.

Mhe. Mwanasheria Mkuu aliwashukuru washiriki wote wa mafunzo na kutoa pongezi kwa wakuu wa taasisi walizotoka kwa kuwaruhusu kuhudhuria mafunzo hayo, huku akiwa na imani kuwa Mawakili wa Serikali walioshiriki mafunzo hayo watakuwa wameelewa vyema Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya Serikali hivyo kuongeza weledi kwenye kazi zao.

# MAWAKILI WAKUMBUSHWA WAJIBU WAO WANAPOISHAURI SERIKALI

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliratibu na kuendesha mafunzo kwa Mawakili wa Serikali hivi karibuni, moja ya mada kuu zilizowasilishwa katika mafunzo hayo ilikuwa ni wajibu wa Wakili wa Serikali wakati wa kuishauri Serikali iliyowasilishwa na Mhe. Jaji George M. Masaju Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mstaafu. Katika mada hiyo Mhe. Masaju alisisitiza Mawakili wa Serikali kuzingatia misingi ya utoaji wa ushauri wa kisheria, uchambuzi wa sera na sheria, ushiriki katika utafiti na uchunguzi na kuzingatia nyenzo za kuhakiki ubora wa nyaraka hizo.

Mhe. Masaju alisisitiza suala la ubora wa kazi za Mawakili wa Serikali, *"ubora wa nyaraka zinazowasilishwa katika Baraza la Mawaziri unaisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi ya kisera na kisheria, hivyo kuchangia katika ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za Serikali na utekelezaji wa sera mbalimbali".*

Katika hatua nyingine Mhe. Jaji Masaju alisema kuwa Wakili wa Serikali ana nafasi kubwa katika mchakato wa maandalizi ya nyaraka za Baraza la Mawaziri, ni muhimu kuhakikisha kuwa nyaraka za Baraza la Mawaziri zinakidhi vigezo vilivyowekwa kulingana na utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za Baraza hilo.

Aliendelea kusema kuwa Wakili wa Serikali ana wajibu wa kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara husika pindi maandalizi ya nyaraka za Baraza la Mawaziri yanapofanyika. Ushauri wa kisheria unapotolewa kwa weledi utaisaidia Wizara husika kuwasilisha nyaraka zilizoidhinishwa kadri inavyohitajika, na zenye misingi thabiti ya kisheria na zinazokidhi vigezo vya Baraza la Mawaziri (BLM). Jukumu hili linajumuisha kuhakikisha Wizara husika inafuata taratibu zote za kisheria na kiutawala na kwamba mapendekezo yaliyomo kwenye nyaraka hizo hayaendi kinyume na Sheria na Sera zilizopo.

Mhe. Masaju aliwakumbusha Mawakili wa Serikali wajibu wao wakati wa nyaraka kwenye Baraza la Mawaziri (BLM). ambapo alisisitiza kufanyika kwa uchambuzi wa akina wa sera na sheria zilizopo ili kubaini mapungufu ya kisheria na kutoa mapendekezo ya maboresho. Ni vyema *"Wakili wa serikali akafanya uchambuzi mzuri kwa minadhili ya kupata ufahamu kwa kina wa sera na sheria zilizopo, athari ya mapendekezo kwa mazingira, gharama na faida inayokusudiwa na jinsi masuala yanayopendekezwa yatakavyoathiri makundi mbalimbali katika jamii kabla mapendekezo hayajawasilishwa mbele ya Baraza".*

Katika hatua za mwisho za uandaaji wa nyaraka hizi, wakili wa serikali anatakiwa kupitia nyaraka kwa makini kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri (BLM) ili kubaini na kuondoa makosa yoyote ya kiufundi na ya uandishi pamoja na uhakiki ubora wa jumla wa nyaraka.

Mafunzo haya yalibainisha makosa na changamoto mbalimbali zinazoathiri ubora wa nyaraka na kuwaalika mawakili wote kushirikiana na wadau mbalimbali wa mchakato huu kwa madhumuni kuzitafutia ufumbuzi wa pamoja. Miongoni mwa changamoto hizi ni pamoja na uzingatiaji hafifu wa mwongozo wa uandishi wa nyaraka za Baraza la Mawaziri (BLM), ushirikishaji hafifu wa wataalamu, hususani katika masuala mahsusi yenye kuhitaji ujuzi maalumu, na ujenzi wa hoja bila utafiti na ushahidi wa kutosha.

# SHERIA ZA KISWAHILI ZITAKAVYOBORESHA HUDUMA ZA KISHERIA

Serikali imedhamiria kuhakikisha sheria zote nchini zinapatikana kwa lugha ya Kiswahili inayoeleweka kwa watu wote. Hayo yamesemwa na Mwandishi wa Sheria Mkuu Msaidizi, Divisheni ya Ufasiri wa Sheria Bw. Said Nzori, wakati akiwasilisha mada katika mafunzo ya siku sita kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Dodoma.

Bw. Nzori alisema kuwa kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura Na.1 inayotaka sheria zote za nchi kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili na kutafsiriwa kwa lugha ya kingereza. Tayari Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetafsiri sheria 210 kati ya sheria 446 za nchi kutoka lugha za kingereza kwenda kiswahili.

Aliongeza kwamba ufasiri wa sheria ni utaratibu unaotumika kubadilisha maandishi ya sheria na nyaraka nyingine za kisheria kutoka lugha moja kwenda katika lugha nyingine kwa kuzingatia kanuni na misingi ya uandishi wa sheria.

Aidha, alibainisha kuwa kuna umuhimu wa kuwepo na tafsiri ya sheria ambayo hurahisisha ujumbe kueleweka kwa ufasaha katika lugha nyingine jambo ambalo lisingewezekana endapo tafsiri isingefanyika. Pia, tafsiri hurahisisha mawasiliano baina ya watu ambao wanatumia lugha tofauti, huimarisha mahusiano baina ya watu na kurahisisha uelewa wa lugha ya sheria.

Vilevile mawakili wa serikali walikumbushwa mambo ya msingi ya kuzingatia katika ufasiri wa sheria ambayo ni pamoja na kuwa na elimu ya sheria, uelewa na weledi katika matumizi sahihi ya misamiati maalum ya kisheria, kuelewa muktadha na madhumuni ya sheria inayotafsiriwa, kuzingatia kila kilicho katika sentensi ya kisheria inayotafsiriwa, kufanya uhakiki wa kutosha, kuzingatia mpangilio wa sentensi ya kisheria, kujua aina ya sentensi iliyotumika.

Pia, Mawakili wa Serikali walifundishw misamiati na alama muhimu katika ufasiri wa sheria na kusisitizwa kwamba ufasiri huzingatia uthabiti na ulinganifu wa lugha ambao unapatikana kwa makubaliano ya matumizi ya baadhi ya misamiati ya kisheria na alama muhimu. Makubaliano hayo yako katika namna zifuatazo; kupitia mazoea, utaratibu wa ndani katika uandishi wa Sheria, na urasimishaji wa misamiati ya kipekee. Kuzingatiwa matumizi sahihi ya Kanuni na taratibu za ufasiri kutawawezesha Mawakili wa serikali kufasiri sheria ndogo na kanuni wanazoziandaa ama kuzitumia katika taasisi zao.

Hata hivyo, Bw. Nzori alielezea changamoto zilizopo katika ufasiri wa sheria ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa mafunzo maalumu juu ya ufasiri wa sheria ndani ya nchi, kukosekana kwa weledi wa kutosha katika matumizi ya lugha ya kiswahili na kingereza kwa baadhi ya watendaji, ufinyu wa bajeti ya kuendesha mazoezi ya ufasiri wa sheria, kukosekana kwa kamusi maalumu za uandishi wa sheria, uwepo wa idadi kubwa ya sheria zinazohitaji kufanyiwa ufasiri.

Mwasilishaji mada alihitimisha kwa kuwasisiiza Mawakili wa serikali kuipenda lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili kwani nchi zote zilizoendelea zinatumia lugha yao kuandika sheria. Kutumia lugha ya Taifa ni nyenzo ya kuendeleza Mamlaka ya nchi dhidi ya ukoloni mamboleo katika mifumo ya sheria ya nchi yetu. Pia, matumizi ya lugha ya Taifa huboresha utoaji wa huduma za sheria na kuimarisha utoaji wa haki kwa wananchi.

# MAWAKILI WA SERIKALI WAPIGWA MSASA KUHUSU MASUALA YA KUZINGATIWA KATIKA MAJADILIANO YA MIKATABA

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Sertikali iliratibu na kuendesha mafunzo kwa mawakili wa serikali, katika mafunzo hayo mojawapo ya mada iliyowasilishwa ni kuhusiana na Masuala ya kuzingatiwa katika Majadiliano ya Mikataba. Mada hiyo ilitolewa na Bw. Hamza S. Johari, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania ambaye pia ni mtaalamu wa masuala ya majadiliano.

Katika wasilisho lake Bw. Johari alieleza kuwa majadiliano ya mikataba yanahusisha muingiliano wa mazungumzo ya kibinadamu wenye ujuzi binafsi na ni lazima Wakili awe na uwezo wa kujenga hoja. Hivyo, alieleza kuwa ili Wakili awe na ubobevu katika majadiliano lazima kuzingatia usikivu wa hali ya juu, uwezo wa kufikiri kwa haraka na hata katika mazingira yaliyokosa utulivu. "*Wakili anapofanya majadiliano ili aweze kufikia muafaka mzuri anapaswa kuwa mwenye shauku ya kujenga hoja na kumudu akili yake kihisia na watu wengine waliopo katika timu ya majadiliano*".

Vilevile, aliwasisitiza Mawakili kuisaidia Serikali katika majadiliano na wanapojenga hoja, lengo liwe ni kufikia masharti bora na mpango mzuri wakiongozwa na msingi wa imani thabiti. Hata hivyo, alieleza umuhimu wa kujiandaa kabla ya kufanya majadiliano kwa kujiuliza maswali magumu ya kubashiri, ili kupelekea kufanya tathmini ya mambo ambayo yanaweza kufanya mazungumzo kwenda vibaya kwa ajili ya kuepusha majadiliano kutofikia muafaka.

Aidha, aliongeza kuwa wakili anapaswa kupata taarifa kamili ya upande wa pili anaofanya nao majadiliano ili kumwezesha kufikia mwafaka stahiki na ni vyema akafahamu eneo la mawanda anayofanyia kazi kama ni sekta ya kibenki, madini, mafuta kwa kuzingatia maslahi na msimamo wa Serikali.

Vilevile Bw. Johari aliendelea kusema kuwa ni muhimu kuwa na uelewa wa muktadha wa soko, mwelekeo wa biashara, viwango vya sekta, miundo ya kifedha, mazingira ya ushindani na mienendo ya kiuchumi ambayo itatoa manufaa kwa timu wakati wa majadiliano.



*Mkurungezi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Bw. Hamza Johari akitoa mada kuhusu masuala ya kuzingatia katika majadiliano ya mikataba katika mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika Jijini Dodoma .*

Bw. Johari alieleza baadhi ya changamoto zinazojitokeza katika majadiliano na mbinu za kuzikabili. Miongoni mwa changamoto hizo ni mazungumzo kuwa na mkwamo, ambapo hakuna upande ulio tayari kulegeza msimamo wake. Unapokabiliwa na changamoto kama hiyo ni muhimu kuweka njia za mawasiliano wazi na kuchunguza sababu ya msingi wa mkwamo huo. Mara nyingi mtazamo mpya au maelezo ya kina zaidi ya msimamo wako yanaweza kusaidia kushinda vikwazo. Changamoto nyingine ni kushughulika na mbinu za msukumo mkubwa wa ushawishi au matakwa yasiyofaa yanayoweza kupelekea makubaliano kutofikiwa, hivyo, Mawakili walishauriwa kuwa na msimamo thabiti wa kutokubali na kusimamia mkakati na malengo ya makubaliano waliyojiwekea.

Mkurugenzi huyo wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, alihitimisha kwa kuwakumbusha Mawakili kuwa, katika nyanja zote za majadiliano Wakili anapaswa kujua ni wapi na jinsi gani anaweza kutoka katika hali ya mkwamo au mvutano huo. Katika mazingira kamahayo mashauriano ya kina na viongozi yanahitajika ili kufanikisha mpango wa majadiliano bila kuathiri malengo. Hivyo ilisisitizwa kuwe na makubaliano katika mijadala hii ikihusisha Ofisi muhimu na mawakili wawe tayari kutumia weledi na ubobevu wao kwa ajili ya kuisaidia serikali kufikia makubaliano.

*Matukio mbalimbali katika picha wakati wa mafunzo maalumu kwa Mawakili wa Serikali*















# TUPO KARIBU YAKO!

**Tufuatilie kupitia**

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora